JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE

Simu. Na 25-2570056
Nukushi. Na. 2570042
Barua pepe:
ded-ileje@iwayafrica.com
mipango@ileje.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 02
ILEJE

Kumb Na.HWI/S.10/16

06/5/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje anawatangazia wananchi wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

Mtendaji wa Kijji Daraja III Ngazi ya Mshahara TGSB (Nafasi 3)

a) Sifa za Mwombaji:-

i) Awe na elimu ya kidato cha nne au sita

ii) Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo:-

- Utawala, Sheria,Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha , Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa, kutoka katika chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

iii) Awe na umri usiozidi miaka 45

b) Majukumu ya Mtendaji wa KijijiDaraja III:-

i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji

ii) Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji

iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipago ya maendeleo ya kijiji

iv) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu

v) Kuandaa taarifa za utelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa , umasikini na kuongeza uzalishaji mali

vi) Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika kijiji , kusimama, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za kijiji.

vii) Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika kijiji

viii) Kupokea , kusikiliza, na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi

ix) Kusimamia utungaji wa Sheria dogo za Kijiji na atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

Mambo Mhimu ya kuzingatia:-

1. Barua za maombi ziadikwe kwa mkono
2. Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyetu vya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa na Picha mbili za rangi (Passport size) za hivi karibuni.
3. Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo binafsi (CV)
4. Kwa waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA)
5. Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe **22/ 05/ 2020** Saa **9.30 alasiri.**

Barua za **maombi zitumwe kwa:-**

Mkurugenzi **Mtendaji (W),**
S.L.P. 2
ILEJE

Haji M. Mnasi
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
ILEJE

KURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA ILEJE